



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA



Dar es Salaam, 12 Julai, 2022

TAARIFA KWA UMMA

MWONGOZO WA NAMNA YA KUFANYA MAFUNZO KWA VITENDO KATIKA VYUO VIKUU VYA NCHINI TANZANIA KWA WANAFUNZI WANAOTOKA KATIKA VYUO VIKUU NJE YA NCHI

1.0 Utangulizi

Kufuatia kuibuka kwa janga la UVIKO-19 pamoja na majanga mengine kama vile vita kati ya nchi ya Urusi na Ukraine, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) imeendeelea kuchukua hatua mbalimbali zenye lengo la kuwawezesha wanafunzi kuendelea na masomo kupitia Vyuo Vikuu vya Tanzania bila kuathiri ubora.

Hatua hizo ni pamoja na kuwekwa kwa Mwongozo wa Taratibu za Uhamisho kwa Wanafunzi wanaotaka kuhamia katika Vyuo Vikuu vya Tanzania (***Credit Accumulation and Transfer Procedures from Foreign Universities to University Institutions in Tanzania***). Mwongozo huu unapatikana katika tovuti ya TCU www.tcu.go.tz.

Vilevile, wapo wanafunzi wanaosoma katika vyuo vikuu vya nje ya nchi ambao wamebakiza mafunzo kwa vitendo (*clinical rotations/field practicals*) na wangependa kufanya mafunzo yao ya vitendo kupitia Vyuo Vikuu vya Tanzania na baadaye kuhitimu mafunzo yao katika vyuo vikuu vya nje ya nchi ambako wanasoma. Wanafunzi hawa

wanatakiwa kutumia utaratibu wa mwanafunzi wa muda mfupi ambao vyuoni hujulikana kwa jina la *occasional student/short-term student*.

2.0 Utaratibu wa kufuatwa kwa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu vya Nje ya nchi Kufanya Mafunzo kwa Vitendo katika Vyuo Vikuu hapa Nchini

Utoaji wa mafunzo kwa vitendo ni sehemu ya mtaala wa masomo wa fani husika. Kwa sababu hiyo, uendeshaji na usimamizi wa mafunzo kwa vitendo ni jukumu la chuo kikuu husika. Mafunzo haya yanaweza kusimamiwa moja kwa moja na chuo kikuu husika au kusimamiwa na chuo kikuu kingine kwa kupitia mashirikiano ya kubadilishana wanafunzi au utoaji wa elimu katika utaratibu wa mwanafunzi wa muda mfupi (*occasional student/short-term student*).

Hivyo wanafunzi waliotoka vyuo vikuu vya nje ya nchi ambao wanataka kufanya mafunzo yao kwa vitendo katika vyuo vikuu vya nchini Tanzania na baadaye kuendelea na masomo yao katika vyuo vikuu wanavyosoma nje ya Tanzania, wanatakiwa kutumia utaratibu wa mwanafunzi wa muda mfupi. Katika utaratibu huu, mwanafunzi anatakiwa kufuata taratibu zifuatazo:

- i). Kabla ya kutuma maombi ya kujiunga na chuo cha hapa nchini kwa ajili ya mafunzo, awasiliane na chuo kikuu cha hapa nchini alichokichagua ili kujua kama kina mashirikiano (*memorandum of understanding*) na chuo kikuu cha nje ya nchi anachosoma;
- ii). Kuhakikisha kuwa anatuma maombi na kujiunga katika chuo kikuu chenye mashirikiano na chuo kikuu chake cha nje ya nchi ili kuwezesha ubadilishanaji wa alama za ufaulu au matokeo ya tathmini zake baada ya kumaliza mafunzo;

- iii). Kuwasiliana na chuo kikuu husika cha hapa nchini ili kujua vigezo mahsusi vya kuzingatia ili kudahiliwa kama mwanafunzi wa muda mfupi; na
- iv). Maombi ya kujiunga na chuo kikuu cha Tanzania kwa ajili ya kufanya mafunzo kwa vitendo yanatakiwa kutumwa moja kwa moja katika chuo kikuu husika.

3.0 Hitimisho

Tume itaendelea kutoa ushauri kwa wanafunzi kwa lengo la kuwawezesha kuendelea na masomo yao hapa nchini kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya uendeshaji wa elimu ya chuo kikuu bila kuathiri ubora wa elimu inayotolewa.

Imetolewa na:



Prof. Charles D. Kihampa

KATIBU MTENDAJI

TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA



Jiandae Kuhesabiwa Siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022